# Jarida la KILIMO

Toleo la Sita
Aprili - Juni, 2011



Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe. Mansoor Yussuf Himid wapili kushoto akipata maelezo kuhusu kilimo cha vanila kutoka kwa mkulima mzoefu wa zao hilo huko katika Kituo Cha Utafiti wa Mazao ya Kilimo, Kizimbani.

## Yaliyomo


Maoni ya Mhariri/ Picha ya Jalada....Uk.2
Ziara ya Rais wa Zanzibar katika maeneo ya Kilimo....Uk.3 - 4
Waziri wa Kilimo akabidhi vifaa vya kupandishia ng'ombe kwa sindano....Uk.5
Waziri wa Kilimo asisitiza utafiti wa mizizi na uhifadhi wa misitu....Uk.6
Uzalishaji wa muhogo Makombeni Pemba....Uk.7
Matukio katika Picha....Uk.8 - 9
Ugawaji wa mbegu za muhogo kwa njia ya vocha....Uk.10
Umwagiliaji maji kwa njia ya matone....Uk.11
Uhifadhi wa misitu ya ukanda wa pwani....12
Utunzaji bora wa kuku wa kienyeji....Uk.13
Upandaji wa minazi ya asili....Uk.14
Faida za kilimo cha Mapesheni ....Uk. 15
Miradi ya Mfuko wa hifadhi ya Jamii TASAF-II....Uk.16

## Bodi ya Wahariri

Washauri
Affan O. Maalim
Juma Ali Juma
Dk. Bakar S. Asseid

Mhariri Mkuu
Dk. Juma M. Akil

Msanifu na Mhariri Mtendaji
Hashim H. Chande

Wahariri Wasaidizi

Makame M. Abdulrahman

Nassor S. Mkarafuu

Othman A. Maulid

Nassor S. Mohammed

Mpiga chapa
Fatma A. Juma

Mpiga picha
Khamis A. Bakari

ANUWANI
Wizara ya Kilimo, Maliasili - Zanzibar
S.L.P. 159
Simu: +255 24 2230986
Fax: +255 24 2234650
E-mail: kilimo@zanlink.com
Tovuti: kilimoznz.or.tz

# MAONI YA MHARIRI

Ndugu Wakulima, umuhimu wa kilimo cha mpunga unaonekana wazi na viongozi wakuu wa Serikali Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Ali Mohamed Shein, Makamo wa kwanza wa Rais Mhe. Seif Sharif Hamad na Makamo wa pili wa Rais Mhe. Seif Ali Iddi katika siku tofauti walipotembelea mabonde ya mpunga yaliyopo katika wilaya na mikoa ya visiwa vya Unguja na Pemba na kujionea wenyewe jinsi kilimo hicho kinavyoendelezwa. Wakati wa ziara zao viongozi hao walipata fursa ya kuzungumza na wakulima na wafanyakazi wa Wizara ya Kilimo na Maliasili na kuweza kujua hali halisi ya kilimo hicho muhimu cha chakula kwa wazanzibari wengi. Ni jambo la fahari kwetu kuona kuwa viongozi wetu hao licha ya kazi zao wana nyingi wameweza kutembelea sekta ya kilimo na kutilia mkazo kilimo hicho na zaidi walifurahishwa na juhudi zinazochukuliwa katika kuimarisha kilimo hicho.

Ndugu Wakulima, hata hivyo ni juu yetu kuongeza bidii katika kuimarisha ukulima wa mpunga kwa kuongeza kasi kwa kutumia mbegu bora, mbolea na kuhakikisha tunapalilia kwa wakati ili mpunga uote vizuri bila ya kuzongwa na magugu. Mara nyingi uzalishaji mpunga huwa duni iwapo hatutotumia mbegu bora, mbolea na kufanya palizi kwa wakati kama inavyoshauriwa na wataalamu.

Ndugu Wakulima, wakati wote wa kuvuna mpunga tunashauriwa kuhakikisha mavuno yetu yanakuwa bora hatuna budi kufuata kanuni bora za uvunaji, uanikaji na uhifadhi wa mpunga wetu. Tukiwa bado katika suala hilo la kilimo cha mpunga inabidi wakulima wa mpunga hivi sasa tufikirie nini cha kupanda baada ya kuvuna mpunga ili tuweze kuongeza kipato chetu, tuhifadhi mashamba yetu kutokana na magugu na kuirutubisha ardhi kwa ajili ya msimu ujao.

Ndugu Wakulima, utafiti uliofanywa unaonesha kuwa katika mabonde ya mpunga wa kutegemea mvua inashauriwa na inandekezwa sana wakulima kupanda kunde baada ya kuvuna mpunga. Kwa mpango huu mkulima anafaidika kwa kupata kunde, kuzuia magugu kuota kwa wingi na kurutubisha ardhi kutokana na zao hilo, hivyo kupanda kunde kunamwezesha mkulima kutengeneza konde yake kwa msimu ujao.

Ndugu Wakulima, mara nyingi baada ya kuvunwa mpunga konde zinaachiwa bila ya kupandwa kitu chochote kunakosababisha kuota kwa magugu na inapofika musimu wa mpunga kazi huwa kubwa zaidi ya kuchimbua na kuburuga.

Ndugu Wakulima, kwa kumalizia ni vizuri tukumbushane kwamba tusijaribu kuuza mpunga wetu wote baada ya kuvuna bila ya kujiwekea akiba, kwanza tuhakikishe tunajiwekea chakula cha kutosha na ziada ndiyo tunaiuza.

# PICHA YA JALADA

Katika picha anaonekana Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe. Mansoor Yussuf Himid akipata maelekezo kuhusu kilimo cha zao la vanila kutoka kwa mkulima mzoefu wa zao hilo huko Kizimbani wakati alipofanya ziara za kuwatembelea wakulima na taasisi zilizomo katika Wizara ya Kilimo na Maliasili.

# ZIARA YA RAIS WA ZANZIBAR KATIKA MAENEO YA KILIMO YA UNGUJA NA PEMBA

Na Mzee M. Mzee

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein alifanya ziara ya kutembelea sekta ya kilimo na maliasili katika visiwa vya Unguja kuanzia tarehe 23 hadi 28/5/2011 na Pemba tarehe 30/5 hadi 4/6/2011. Ziara hiyo ilikuwa na lengo la kujua mafanikio, changamoto na hatua za kuwasaidia wananchi kufikia malengo ya Serikali ya kujitosheleza kwa chakula, lishe na kupunguza umasikini nchini. Katika ziara hiyo Mhe. Rais aliongozana na Mhe. Mansoor Yussuf Himid Waziri wa Kilimo na Maliasili, Katibu Mkuu, Manaibu Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na Maofisa wa Wizara hiyo.

Ziara hiyo ilianza kwa kukagua kilimo cha mpunga wa umwagiliaji maji katika bonde la Mtwango ambapo aliwaahidi wakulima kuwapatia pembejeo kwa bei nafuu na kwa wakati na kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji maji na kusisitiza kuwa kilimo bila maji, mbolea na mbegu bora hakiwezi kuwa na tija.

Akiwa katika Bonde la Bumbwisudi Mhe. Rais alipata maelezo ya mafanikio, changamoto na malengo ya uzalishaji wa mpunga na aliahidi kuzipatia ufumbuzi changamoto zilizopo na kusema Serikali ina nia ya kumkomboa mkulima ili aondokane na kilimo duni na kufikia kilimo chenye tija kwa faida yake na kwa taifa.

Katika Kituo cha Kilimo Kizimbani Mhe. Rais alitembelea sehemu ya utafiti wa mbegu za mpunga, muhogo na migomba na kupata maelezo ya uzalishaji wa mbegu na utafiti wa udhibiti wa wadudu na maradhi, ambapo aliombwa kusaidia vitendea kazi na kaboresha maslahi ya watafiti waliopo ili wasikimbie kutokana na maslahi duni.

Akiwa katika sehemu ya utibabu wa mimea na ukaguzi wa mazao,Mhe. Rais alipata maelezo kuhusu udhibiti wa nzi wa matunda, kuangalia maabara ya uzalishaji wa miche kwa kutumia Chupa (Tissue culture) na maabara ya udongo ambapo alionyeshwa aina tofauti za udongo zilizopo Zanzibar na kupata maelezo juu ya utafiti wa udongo na faida zake kwa mazao. Pia alitembelea kituo cha usarifu wa mazao na kushauri jambo hili lipewe kipaumbele na



Raisi wa Zanzibar, Mhe: Dkt. Ali Mohamed Shein wa kwanza kulia akiwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo na Maliasili ndugu Affan O. Maalim na wafanyakazi wengine akipata maelezo kuhusu kilimo cha umwagiliaji maji kutoka kwa mtaaamu ndugu Kadiri

kuwashajiisha wawekezaji wa ndani kuwekeza katika sekta hiyo. Aidha, aliwataka wafanyakazi na wanafunzi wa Chuo cha Kilimo Kizimbani kusoma zaidi na kwa bidii na kuahidi kukisaidia chuo hicho kiweze kutoa Diploma hadi Digirii.

Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein katika Mkoa wa kusini Unguja, alimtembelea ndugu Ahmed Saleh mkulima mwekezaji wa shamba la viungo na matunda hapo Kidimni, Kituo cha Uzalisha mbegu za kilimo Bambi kuangalia uzalishaji na utayarishaji wa mbegu mpya za mpunga aina ya NERICA, pia alifika bonde la mpunga Cheju na kukagua ukulima wa mpunga wa kutegemea mvua. Aidha, Rais aliwatembelea wakulima wa migomba pamoja na shamba la migomba la Mwakilishi wa Jimbo la Makunduchi, Mhe. Haroun Ali Suleiman na alimalizia ziara yake kwa kufanya majumuisho katika ukumbi wa Chuo Kikuu cha Zanzibar Tunguu.

Mhe. Rais akiongozana na Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe. Mansoor Yussuf Himid pamoja na mawaziri wengine, wakuu wa mikoa, makatibu wakuu na viongozi wa vyama vya siasa alifanya ziara kama hiyo kisiwani Pemba. Akiwa katika Wilaya ya Wete alitembelea Kituo cha kilimo cha mpunga wa umwagiliaji maji Mangwena na kupata maelezo ya utekelezaji wa kilimo hicho. Katika shamba la ushirika la Mabibo Junguni Mhe. Rais alipata fursa ya kuangalia kilimo cha mikarafuu, muhogo na mdalasini ambapo alieleza kuwa Serikali ina mpango maalum wa kuimarisha zao la karafuu na kupunguza bei za pembejeo, pia aliiagiza Wizara ya Kilimo na Maliasili kuandaa ziara za wakulima kutoka maeneo mbali mbali ya Zanzibar kwenda huko kujifunza kilimo cha mikarafuu.

Ziara iliendelea katika Wilaya ya Micheweni kwa kutembelea bonde la Kanambe kwa kukagua ukulima wa mpunga, kupata maelezo ya ukulima huu na changamoto zilizopo ikiwa ni pamoja na kutotumia mbegu bora, matumizi madogo ya mbolea na upungufu wa mvua katika kipindi cha kuchanua mpunga. Mhe. Rais alihimiza kulima kilimo chenye tija na kuwataka wakulima waongeze juhudi ili kuzalisha angalau gunia 30 hadi 40 za mpunga kwa eka na Serikali itajitahidi kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji maji.

Katika bonde la Mpunga la Mziwanda ambalo linategemewa na watu wengi wa Micheweni kwa kilimo hicho, kuingiliwa na maji chumvi Rais alishuhudia. Mhe. Rais akiangalia

madhara hayo ambayo yameathiri kwa kiasi kikubwa kilimo cha mpunga, aliagiza kujengwa kizuizi katika eneo hilo kama ilivyofanyika katika maeneo mengine. Wakulima nao walimuomba Mhe. Rais kuwasaidia ujenzi wa tuta la zege, kuwapatia mbegu bora, mbolea na huduma za matrekta.

Katika Shamba la Mtama lililopo Mjini Wingwi, wakulima walimlalamikia Mhe. Rais kutokutekelezwa kwa ahadi yake aliyoitoa mwezi Februari ya kuwapatia mbegu bora ya mtama ambapo kulisababisha wakulima kutumia mbegu za kienyeji. Nae Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo alieleza kuwa mbegu tayari zimeshanunuliwa na ilishindikana kuigawa kwa sababu wakulima walikuwa wamekwisha panda. Hata hivyo, Mhe. Rais aliagiza mbegu hiyo ipelekwe kwa wakulima ili waitunze wenyewe na Wizara ya Kilimo na Maliasili tayari imetekeleza agizo hilo.

Ziara ya Mhe. Rais iliendelea siku ya nne kwa kupokea taarifa ya Mkoa Kusini Pemba ambayo ilisomwa na Mkuu wa Mkoa, ambapo alifika bonde la Kichwa ambalo lina jumla ya ekari 20 na wakulima 46, ambapo alipata maelezo mafupi. Naye Waziri wa Kilimo na Maliasili aliahidi kuwa Serikali itaongeza usambazaji wa taaluma na wataalamu wa kilimo kwa kuajiri mabwana/mabibishamba 110" na kuwashauri wakulima kuunda Jumuia ili kurahisisha upatikanaji wa huduma hizo.

Rais pia alifika katika bonde la mpunga Kimbuni lenye wakulima 67, ambalo lilianza kilimo cha umwagiliaji maji mwaka 1979 katika hekta 6. Wakulima nao walimueleza Mhe. Rais kilio chao kinachorejesha nyuma jitihada zao za kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji kunakopelekea kupata mavuno madogo ikiwa ni pamoja na ukosefu wa mabwanashamba na bei kubwa za pembejeo.

Mhe. Rais aliendelea na ziara katika kijiji cha Sanani kwa kuangalia athari ya uharibifu wa mazingira iliyotokana na uchimbaji wa matofali ambako aliwasihi wananchi kuachana na uharibifu huo na kuagiza mashimo hayo yapandwe miti. Huko Makombeni

Mhe. Rais aliangalia kilimo cha mpunga wa umwagiliaji maji na kupata maelezo ya mradi unaofadhiliwa na JICA, Serikali na wananchi. Wakulima wa hapo walimuomba Mhe Rais kusaidia ujenzi wa bara bara ya lami yenye urefu wa kilomita mbili katika maeneo ya Mbuguani, Uweleni na Ng'ombeni ili kurahisisha usafirishaji wa mazao ya karafuu, mpunga na pembejeo hasa wakati wa mvua.

Katika Wilaya ya Chake Chake Mhe. Rais alitembelea bonde la Mfubaha huko Vitongoji ambalo hutumika kwa kilimo cha mpunga wa kutegemea mvua, bonde hilo lina ukubwa wa ekari 100 na kwa msimu huu asilimia 90 ya ekari hizo zililimwa. Wastani wa mavuno kwa sasa ni kilo 600 kwa eka wakati upo uwezekano wa kupata tani 2.8 kwa eka. Mbali na maelezo aliyoyapata kutoka kwa wakulima na changamoto zinazosababisha uzazi duni zikiwemo ukosefu wa mvua za kutosha na matumizi madogo ya mbolea na upungufu wa mabwanashamba. hivyo wakulima waliomba waongezewe mabwanashamba kwani mmoja aliyopo hatoshi na waundiwe taasisi itakayo simamiwa na wakulima kufuatilia kilimo.

Mhe. Rais alitembelea Skuli ya Wakulima wa Muhogo Dodo Pujini na kuwaambia wakulima kuwa Serikali itawapatia huduma za matrekta na pembejeo na inawataka walime kilimo cha kisasa chenye tija.

Mhe. Rais aliwashukuru viongozi na wananchi walioshiriki katika ziara hiyo Unguja na Pemba. pia alifurahishwa na juhudi za wakulima katika maeneo aliyoyatembelea. Katika ziara hiyo aliagiza kuangalia uwezekano wa kusarifu mazao ya mashelisheli, ndizi na muhogo ambayo yanapatikana kwa wingi hapa visiwani ili kupata soko. Pia aliitaka Wizara ya Kilimo kulitafutia ufumbuzi suala la uhifadhi wa chakula ili kuhakikisha usalama na uhakika wa chakula Zanzibar.

Mhe. Rais aliitaka Wizara ya Kilimo na Maliasili kwenda sambamba na azma ya Serikali ya kuimarisha kilimo hivyo kufikisha taarifa za kitaalamu kwa wakulima na kwa wakati. Aidha, aliwataka watendaji kuwa wazi, wakweli, wabunifu na kuwatembelea wakulima badala ya kutumia muda mwingi maofisini.

Mhe. Rais alisema Serikali imedhamiria kutoa kipaumbele kwa zao la karafuu pamoja na kufanya utafiti utakaoongeza thamani ya karafuu na mazao mengine ya viungo. Aidha, aliitaka Wizara ya Fedha kutoa Shillingi millioni 14.5 kwa ajili ya kurekebisha mashamba yaliyoharibika kwa kujaa mchanga wakati wa ujenzi wa barabara ya Wete – Gando huko Mangwena na kuahidi kuchangia Shilingi milioni mbili (2,000,000/=) ili kuimarisha ushirika wa Mabibo Junguni.

Mhe. Rais aliahidi kuwapatia ardhi kikundi cha wakulima wa muhogo cha Mitamani Pujini ambapo Wizara ya Biashara imeahidi kukipatia gari dogo la mizigo (pick-up) na Wizara ya Ushirika imeahidi kutoa gari la matairi 3 (bajaj) ili kurahisisha usafirishaji wa mazao yao.

MAPINDUZI YA KILIMO NCHINI ni kauli mbiu inayohusisha dhana nzima ya kuendeleza kilimo na kupatikana kwa uhakika wa chakula. Hivyo wananchi wametakiwa kufanyakazi kwa bidii.



Raisi wa Zanzibar, Mhe: Dkt. Ali Mohamed Shein wa tatu kushoto akiwa na viongozi wengine wa Serikali alipata fursa ya kuangalia kilimo cha Karafuu na kuzungumza na wakulima wa zao hilo huko Pemba.

# VIFAA VYA KUPANDISHIA NG'OMBE KWA SINDANO VYAKABIDHIWA

Na Hashim H. Chande

Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe. Mansoor Yussuf Himid kwa niaba ya Wizara hiyo alikabidhi vifaa vya upandishaji ng'ombe kwa njia ya sindano vyenye thamani ya shilingi 60,884,236.00 kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Said Ali Mbarouk kwa ajili ya kusaidia Sekta ya Mifugo. Makabidhiano hayo yalifanyika tarehe 28/04/2011 katika ukumbi wa Programu za Kuimarisha Huduma za Kilimo na Mifugo (ASSP/ASDP-L) Maruhubi.

Baada ya makabidhiano hayo Mhe. Waziri aliinasihi Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuvitunza na kuvitumia vizuri vifaa hivyo na kwa malengo yaliyokusudiwa, Ili vitumike kwa muda mrefu na kuipunguzia Serikali gharama kubwa za kununua vifaa kama hivyo.



Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe. Mansoor Yussuf Himid wapili kulia akimkabidhi vifaa vya upandishaji ng'ombe kwa njia ya sindano Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Said Ali Mbarouk wapili kushoto

Mafanikio ya program hizi katika kutoa taaluma bora kwa wakulima na wafugaji kutokana na kazi wanazozifanya ndio mwanzo wa Mapinduzi ya Kilimo Visiwani, kwa kuwa chanzo cha maendeleo ya kitu chochote ni elimu ambayo ndio kipengele kikubwa cha Programu hizi

Vifaa ambavyo vilitolewa kupitia Programu za ASSP na ASDP-L ni kama vinanyoonekana katika jaduweli lifuatalo:

Waziri alieleza kwamba Program hizi mbili za kutoa huduma za kilimo na mifugo zinawajengea uwezo wakulima na wafugaji wetu kutambua matatizo yao, kutoa kipaumbele cha matatizo na kuyapatia ufumbuzi kulingana na rasilimali zilizopo.

Aidha, alifahamisha kwamba katika juhudi za kuimarisha sekta ya mifugo Programu ya Kuendeleza Huduma za Mifugo (ASDP-L) iko mbioni kukamilisha ukarabati wa vituo vya kutoa huduma za afya ya mifugo, uzalishaji na maabara zake. Vituo hivyo ni pamoja na Konde, Kengeja, Mangapwani na maabara za mifugo zilizopo Maruhubi na Chake Chake. Kwa sasa mkataba wa ukarabati wa chinjio la kisakasaka upo tayari na mkandarasi ameshatia saini na ujenzi unategemewa kuanza hivi karibuni ambapo jumla ya shilingi 191,803,766.00 zimetengwa na program mwaka huu kukidhi ukarabati wa majengo na ununuzi wa vifaa vyake ili viweze kutoa huduma zinazostahili.

| S.No | Description | Unit | Gty |
|---|---|---|---|
| 1. | Artificial vagina | set | 4 |
| 2. | Rough latex liners for AV | set | 4 |
| 3. | Rough neoprene liners for bovine | set | 4 |
| 4. | Smooth neoprene liner for bovine | set | 4 |
| 5. | Smooth latex liners for AV | set | 4 |
| 6. | Reusable cones for Bovine AV | dozen | 4 |
| 7. | Reusable Protective cover for AV | dozen | 4 |
| 8. | Pyrex 15ml Graduated tubes | dozen | 4 |
| 9. | Gumboots | Pair | 6 |
| 10. | Liboratory coats | pcs | 6 |
| 11. | Overall | pcs | 6 |
| 12. | Digital thermometer | pcs | 2 |
| 13. | Semen extender | bottle | 6 |
| 14. | Micros cope | Pcs | 1 |
| 15. | AI kit | Kit | 50 |
| 16. | Insemination sheath | packet | 20 |
| 17. | Infrared sterilizer | Pcs | 1 |
| 18. | Water bath (with regulated temperature | Pcs | 1 |
| 19. | GnRH | Vial | 6 |
| 20. | Gonadotrophin | pack | 6 |

# WAZIRI WA KILIMO NA MALIASILI ASISITIZA TAFITI ZA MAZAO YA MIZIZI NA UTUNZAJI WA MISITU

Na Sabiha K. Ahmed

Katika kuendeleza juhudi za wakulima wa zao la muhogo, Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe. Mansoor Yussuf Himid alifanya ziara ya kutembelea wakulima wa muhogo katika kijiji cha Machui Wilaya ya Kati Unguja ambako aliwataka wakulima kuwa na matarajio makubwa ya mabadiliko katika sekta ya Kilimo katika Bajeti ya mwaka huu 2011/2012.

Alieleza kuwa Wizara imekusudia kufanya utafiti zaidi wa mazao ya mizizi, hatua ambayo itakuza kilimo cha mazao hayo na kuwaongezea kipato wakulima. Aidha, Waziri aliwataka wakulima hao kuongeza juhudi na kutokata tamaa kwa gharama kubwa za pembejeo na Serikali tayari imezingatia mahitaji yao.



Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe; Mansoor Yussuf Himid akiangalia shamba la mkulima wa muhogo ndugu Khamis Mkubwa wa Kichunjuu Pembe alietumia mbegu bora aina ya Kizimbani iliyotolewa na Kituo cha Utafiti wa Kilimo Kizimbani.

Nae ndugu Suleiman John, mkulima wa muhogo katika kijiji cha Machui alimueleza Waziri wa Kilimo na Maliasili kuwa walikuwa wanakabiliwa na tatizo la upatikanaji wa mbegu ya muhogo kwa muda mrefu baada ya mbegu zao za asili kuathiriwa na maradhi ya kansa ya muhogo na hivi sasa tatizo hilo limetatuliwa na Wizara ya Kilimo baada ya kufanya utafiti na kupatikana kwa mbegu mpya nne za muhogo aina ya Mahonda, Machui, Kama na Kizimbani ambapo mbegu ya Machui inastawi vizuri katika kijiji hicho.

Mhe. Mansoor akiwa katika ziara ya kutembelea Msitu wa Kiwengwa-Pongwe aliwataka wanakijiji kuwa na mtazamo wa ulimwengu unaolenga zaidi katika uhifadhi na utunzaji wa rasilimali ya misitu na kujua kwamba misitu humkomboa binaadamu kwa kumpatia kipato na kuongeza pato la Taifa. Aliwafahamisha wanakijiji hao alisema ili nchi iweze kunufaika kutokana na misitu, jamii inapaswa kuendeleza ushirikiano katika jitihada za kuhifadhi misitu isipotee.

Hifadhi ya Msitu wa Kiwengwa-Pongwe ni ya pekee, yenye thamani na ni ya pili kwa ukubwa katika ukanda wa Kaskazini Unguja kwa kuzalisha kuni, mkaa na dawa za asili. Msitu huu ni rasilimali muhimu unaochangia pato la Taifa na ni chanzo kikuu cha mvua na una mapango ya maji ambayo ni chanz cha maji ya uhakika kwa matumizi ya mahoteli ya Ukanda wa Pwani ya Kiwengwa. Hivyo amewataka wananchi kuitunza rasilimali hiyo ili iendelee kuinufaisha nchi na kuimarisha ustawi wa maisha yetu.

Lengo kuu la hifadhi ya msitu huu ni kuimarisha utalii na kukuza mfuko wa hazina ya Serikali. Katika kuhakikisha msitu huo unavutia kiutalii. Waziri alisisitiza kuwa ipo haja kwa wawekezaji kuwekeza ndani ya msitu huo, kinachosubiriwa ni kukamilika kwa taratibu za kisheria.

Uhifadhi wa Msitu wa Kiwengwa-Pongwe unakabiliwa na changamoto za ukosefu wa vitendea kazi pamoja na uvamizi hivyo wananchi wameshauriwa kuongeza za msitu huo na kwamba Serikali iko pamoja nao.



Sehemu ya msitu wa hifadhi ya Masingini unaokabiliwa na uharibifu mkubwa hivi sasa ambao ni chanzo kikuu cha maji yanayotumika na wakaazi wa Mjini.

# MAKOMBENI YAONGEZA UZALISHAJI WA MUHOGO

Na Shauri Haji

Muhogo ni zao la chakula linalolimwa na wakulima wengi katika visiwa vya Unguja na Pemba na inakisiwa jumla ya ekari 75,000 hulimwa zao hili ambapo wastani wa tani 152,751 huzalishwa kwa mwaka kwa ajili ya chakula na biashara. Hata hivyo inakadiriwa asilimia 90 ya wakulima wa Zanzibar hulima muhogo katika misimu ya Masika na Vuli.

Bwana Juma Saidi Moh'd mwenye umri wa miaka 42 ambaye ni Katibu wa Skuli ya Wakulima "Tuko Fit" Shehia ya Makombeni, Wilaya ya Mkoani Pemba ni miongoni mwa wakulima wa muhogo aliyepata mafunzo ya upandaji wa muhogo na kutumia mbolea ya samadi kupitia Programu za Kuimarisha Huduma za Kilimo na Kuendeleza Sekta ya Mifugo (ASSP&ASDP-L).

Kutokana na mafunzo hayo ndugu Juma alipata mafanikio makubwa yaliyompelekea kuwa mhamasishaji wa zao la muhogo kwa kuwashauri wakulima wenzake wakati wa kupanda, kutumia mbegu zilizofanyiwa utafiti, ukataji wa mbegu, urefu wa mbegu unaostahiki na upandaji ili kudhibiti uharibifu, kuongeza mavuno na tija kwa mkulima.

Alishauri wakati wa kupanda kisiki cha muhogo kinatakiwa kiwe robo au nusu yake kifukiwe chini ya udongo ili kurahisisha kung'oa na kama kitapandwa kwenye ardhi ya kichanga kiingizwe hadi robo tatu. Palizi ya kwanza ifanywe wiki moja na nusu au mbili baada ya kupandwa na ya pili baada ya miezi miwili kutegemea uotaji na ukuaji wa magugu. Mpaka sasa ndugu Juma ametoa taaluma hiyo kwa wakulima wenzake 100, wakiwemo wanawake 30 na wanaume 70 katika Wilaya hiyo.



Juma Saidi Mohd mkulima wa muhogo wa Makombeni, Mkoani, Pemba akiwa katika konde yake ya muhogo

Kutokana na kutumia mbegu bora za muhogo za kisasa aina ya Mwari, Mahonda, Machui na Kizimbani, mkulima huyo alisema uzalishaji umeongezeka katika Shehia hiyo tofauti na mbegu za zamani ambazo zikitoa mavuno kidogo kufuatia kukumbwa na maradhi ya michirizi na Mosaic ambayo yaliangamiza mbegu za Boma, Mdonge, Hameni mjini Kigoma na Jawa na kumsababishia wakulima kupata mavuno hafifu na kuongeza umasikini.

Mbegu hizo mpya za muhogo zinatoa mavuno ya wastani wa kilo nne hadi tano kwa shina na shina moja lina thamani ya shilingi 3000/= hadi 4000/= . Kutegemea na msimu. Mbegu za Mahonda na Machui ndizo zinazostawi zaidi katika Shehia ya Makombeni kwani shina moja na huweza kutoa wastani wa kilo tano na nusu.

Hata hivyo, changamoto zilizopo ni maradhi aina ya ukungu na michirizi ambayo hushambulia na kuangamiza mbegu za Boma, Mdonge, Hameni Mjini, Mbega na Kigoma. Changamoto nyengine ni pamoja na ukosefu wa maeneo kwa ajili ya utanuzi wa mashamba.

Kutokana na Changamoto hizo huduma za mbegu bora hutolewa na Wizara ya Kilimo na Maliasili kupitia Taasisi zake za Utafiti wa Kilimo na Elimu kwa Wakulima kwa kutumia shamba darasa kwa kuwapa mafunzo na kuwajengea uwezo wakulima ili kuongeza uzalishaji wenye tija.



Muhogo uliopatikana kwa kutumia taaluma bora na ushauri wa kitaalamu.

# Matukio ka



Raisi wa Zanzibar, Mhe: Dkt. Ali Mohamed Shein wa katikati akiwa na Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe; Mansoor Yussuf Himid kulia kwake akipata maelezo kuhusu uzalishaji wa mbegu ya mpunga aina ya NERICA kutoka kwa Ndugu Affan O. Maalim, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo na Maliasili katika kituo cha uzalishaji wa mbegu Bambi.



Raisi wa Zanzibar, Mhe: Dkt. Ali Mohamed S
linaloendelea kujengwa la kituo cha mafunzo
maelezo yake kutoka kwa mkuu wa mradi hu
ziara ya kukitembelea kituo cha Utafiti wa kilim



Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe. Mansoor Yussuf Himidi kushoto akipokea msaada wa darubini ambayo itatumika katika uchunguzi wa mbegu kutoka kwa aliyekuwa Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) Tanzania Dk. Louise L. Setshwaelo wakati alipofika Wizarani kumuaga baada ya kumaliza muda wake hapa nchini.




Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe: Mansoor Y
'Jahazi' aliyekuwa Mwakilishi Mkaazi wa Shirika
Dkt. Louise L. Setshwaelo wakati alipofika Wiz
hapa nchini, kushoto na Mkurugenzi wa Sera, M

# atika Picha



Shein kushoto akiangalia mchoro wa jengo ya usarifu wa mazao ya kilimo na akipata o Ndugu Saleh M. Juma, wakati alipofanya no Kizimbani.



Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Ushirika, Mhe; Haroun Ali Suleiman mwenye suti nyeupe akiangalia na kupata maelezo kuhusu mpunga uliozalishwa kwa mbegu ya NERICA kutoka kwa Mkurugenzi wa Kilimo ndugu Mberek Rashid huko katika viwanja vya Amani baada ya kuyafungua rasmi maonyesho ya siku ya wafanyakazi duniani (Mei mosi).



Yussuf Himid katikati akimkabidhi zawadi ya la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) Tanzania arani kuaga baada ya kumaliza muda wake Mipanga na Utafiti Dkt. Juma M. Akil.



Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe: Mansoor Yussuf Himid kulia akipata maelezo kuhusu kilimo cha uyoga na viungo kutoka kwa mtaalamu wa mazao hayo ndugu Foum Ali Garu katika viwanja vya Amani wakati wa maonyesho ya siku ya wafanyakazi duniani (Mei mosi) alipotembelea banda la Wizara ya Kilimo na Maliasili.

# UGAWAJI WA MBEGU ZA MUHOGO KWA VOCHA

Na Haji H. Saleh

Wizara ya Kilimo na Maliasili kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar imeanzisha huduma ya Vocha kwa ajili ya ugawaji wa mbegu za muhogo. Vocha ni karatasi maalum yenye thamani ya fedha na hutumika kwa ajili ya upatikanaji wa mbegu na pembejeo kwa wakulima wasio na uwezo wa kununua na kupata pembejeo husika.

Hapa Zanzibar, mfumo huu wa vocha ulianza kutumika kwa majaribio katika vijiji vya Mahonda, Machui, Makunduchi, Uzi na Kisauni ambako ulilenga kutoa fursa kwa wakulima wasio na uwezo wa kununua mbegu mpya na bora za muhogo zenye uzazi mkubwa na kustahamili maradhi.



Mkulima akitayarisha mbegu ya muhogo aina ya Kizimbani kwa ajili kuzitoa kwa wakulima wenzake kwa mfumo wa vocha

**MAFANIKIO YALIYOPATIKANA**

Katika awamu ya kwanza ya majaribio jumla ya wakulima 1,217 walifaidika, hasa wale walioharibikiwa na mazao yao kutokana na majanga ya maradhi ya muhogo yanayosababishwa na virusi (Cassava Brown Streak Disease, CBSD, na Cassava Mosaic Disease, CMD). Hata hivyo, imebainika kuwa wakulima wengi hawana uwezo wa kununua mbegu bora kutoka kwa wazalishaji wa mbegu hizo.

**MAMBO YA KUFUATA WAKATI WA KUSHAJIISHA MATUMIZI YA VOCHA**

i. Kuandaa mkutano na kushajiisha viongozi wa Wilaya, Shehia na Vijiji husika kwa lengo la kutoa uwelewa na umuhimu wa mfumo wa vocha,

ii. Kutumia vigezo maalum ikiwa ni pamoja na “PRA wealth ranking tool” kwenye jamii (shehia) zitakazohusika na zoezi hili ili kupata watu wanaostahiki kupata msaada au huduma hii kwa mujibu wa uwezo wao,

iii. Kutayarisha orodha ya wazalishaji wa mbegu bora ambazo zinatumika katika usambazaji kwa kutumia vocha,

iv. Kuandaa mpango wa kuwatembelea wazalishaji mbegu na kuangalia ubora wa mbegu zinazozalishwa ili kuepuka usambazaji wa mbegu zisizo na viwango,

v. Kusambaza orodha ya wenye mbegu kwa wakulima wanaotegemewa kupata mbegu hizo ili wafahamu muda na wapi wakachukue mbegu hizo baada ya kukabidhiwa vocha zao,

vi. Kutayarisha mkutano wa wanaotarajiwa kupata vocha na kuzigawa vocha katika mazingira ya uwazi na ukweli.


vii. Kuwashirikisha viongozi wa ngazi husika ili kila mdau aelewe hatua zinazoendelea katika eneo lake,

viii. Kufanya mkutano na wazalishaji wa mbegu na kuwaelezea taratibu za ugawaji wa mbegu na namna watakavyopata malipo yao baada ya kubadilishana vocha na mbegu,

ix. Kubadilishana vocha na mbegu,

x. Kuchukua takwimu za vocha zilizotolewa sambamba na kufanya malipo kwa wazalishaji mbegu. Kila vocha moja ya muhogo ina thamani ya shilingi 3000/= ambayo ni sawa na thamani ya mzigo mmoja wa mbegu mpya.

xi. Kila mkulima aliyeteuliwa amefaidika na mpango huu kwa kupata si zaidi ya vocha mbili zenye thamani ya shilingi 6000/=



Kizimbani Agric. Research Institute
Ministry of Agriculture and Natural Resources
Root and Tuber Crops Research Unit
P.O Box 159 Zanzibar

*Kwa mazao mengi ya muhogo, daima tumia na chagua mbegu za muhogo zinazotokana na mimea inayostahamili magonjwa ya batobato (CMD) na kansa ya mihogo (CBSD)* — Namba ya vocha

Jina la mmiliki wa Vocha
(Voucher holder)________ Tarehe________

Wilaya________ Shehia________ Saini________

Jina la muuzaji wa mbegu
(Vendor)________ Tarehe________

Wilaya________ Shehia________ Saini________

*Vocha hii ina thamani ya TSh 3000/= na inaweza kutumika ndani ya siku 30 tu kuanzia tarehe ya kutolewa*

| Na | Aina ya mbegu ya muhogo | Idadi ya mbegu | Maoni |
|---|---|---|---|
| 01 | | | |
| 02 | | | |
| 03 | | | |

Vocha hii imetolewa na
________ Saini________

Cheo________ Tarehe________
*Muhuri wa Idara/Sehemu inayohusika*

Mfano wa vocha inayutumika kupata mbegu za mihogo.

xii. Mzalishaji mbegu hukusanya vocha zake na kuzipeleka katika Kitengo cha Utafiti wa Mazao ya Mizizi kwa malipo kila mwisho wa mwezi,

xiii. Ili vocha iweze kulipwa lazima ionyeshe sahihi za wahusika akiwemo mtoa vocha, Mkuu wa Kitengo, mzalishaji mbegu pamoja na tarehe ya mabadilishano hayo (Kama inavyoonekana kwenye sampuli ya vocha),

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA MATUMIZI YA VOCHA**

- Uwekaji kumbukumbu kwa wazalishaji mbegu nzuri na zenye viwango vinavokubalika.
- Kutoa taaluma kwa washiriki wote kuhusu utaratibu wa vocha.
- Uchaguzi wa wanufaika na huduma hii lazima waachiwe wanajamii wenyewe ili kuepuka malalamiko kwa wataalam kuwaingilia na kutoa upendeleo kwa baadhi ya watu

**FAIDA ZA MATUMIZI YA VOCHA**

Mfumo huu umesaidia wakulima katika nyanja nyingi, ikiwemo kuenea kwa mbegu bora zinazozalishwa katika vituo vya utafiti na kwa wazalishaji wa mbegu, kuwapatia mbegu bora wakulima wasio na uwezo wa kununua mbegu kutoka kwa wazalishaji. Kupata mafunzo juu ya matumizi ya vocha na kubadilishana uzoefu katika uzalishaji wa mazao na kuwapatia soko wazalishaji wa mbegu.

**HITIMISHO**

Mfumo wa matumizi ya vocha katika ugawaji wa mbegu za muhogo umeonesha kwamba unaweza pia kutumika katika ugawaji au utoaji wa huduma kwa mbegu za mazao mengine na pembejeo za aina tofauti. Kutokana na uzoefu uliopatikana inashauriwa juhudi zaidi zichukuliwe ili kupanua matumizi ya mfumo wa vocha.

# UMWAGILIAJI MAJI KWA MATONE

Na Amour Uzzi

Umwagiliaji kwa njia ya matone ni utaratibu wa kumwagilia maji taratibu kwenye udongo kwa kutumia chombo kilichotayarishwa kwa kunyunyizia maji kwenye sehemu iliyochaguliwa kufuata mistari inayotoa maji. Vinyunyizo hivi huwekwa juu ya ardhi lakini pia vinaweza kufukiwa ndani ya ardhi.

Umuhimu wa umwagiliaji maji kwa njia ya matone ni kuhakikisha maji hayapotei kwa wingi na yanapenya vizuri ndani ya ardhi na husaidia kupunguza na kuyayusha chumvi kwenye mmea na magugu pia hupungua. Mbolea na madawa yanaweza kutumika moja kwa moja kwa kutia ndani ya maji na kupelekwa kwenye mmea. Mfumo huu hupunguza gharama na kuajiri vibarua wengi shambani na gharama. Huokoa upoteaji wa maji kwa asilimia 50 na hutumika zaidi kwenye sehemu zenye uhaba wa maji.

Licha ya faida za umwagiliaji maji kwa njia ya matone pia zipo hasara chache kama vile, kuziba vinyunyizo mara kwa mara na husababisha maji yamwagike vizuri kwenye mimea. Gharama za kuanzia huwa kubwa ambapo wakulima wadogo wadogo wanashindwa kuzimudu.

Hapa Zanzibar umwagiliaji maji kwa njia ya matone unaendelea kukua siku hadi siku na Mkoa wa Mjini Magharibi unaongoza kwa kuwa na watu wengi wanaotumia mfumo huo ukifuatiwa na Mkoa wa Kusini Unguja. Aidha, umwagiliaji kwa njia ya matone



Umwagiliaji kwa njia ya matone huimarisha mboga mboga na kumuwesha mkulima kupata mavuno wakati wote wa msimu

umegawika katika sehemu kuu tatu kama zifuatazo:

**Umwagiliaji katika bustani za majumbani**

Vifaa na vitu muhimu vinavyohitajika kwenye mfumo wa umwagiliaji ni pamoja na vianzio vya maji (kisima, mto, ziwa, bwawa au maji yanayotuama), pampu ya kusukumia maji kuingiza tangini, jenereta au umeme, mipira ya ¾ au ya inchi 1 na viungo vyake. Micro Drip 1.9L/H o.3M 250M, Ental Pungers/F4/7F.D, Ental Coller F.D (0.5-2001), AM 1" Super Disc Filter 120, Quick all Punch 3mm Plastic Narrow Teflon na Connector for Micro Drip/Landli.

**Umwagiliaji wa matone kwenye mashamba makubwa.**

Mashamba makubwa yanahitaji mipira mikubwa ya maji ikilinganishwa na ile ya umwagiliaji katika bustani za majumbani.

**Umwagiliaji wa matone kwa chupa**

Njia hii inafaa kutumika zaidi katika miti mikubwa ambayo inahuishwa mashambani.

**Angalizo**

Tangi au sehemu ya kuhifadhia maji inatakiwa iinuke kwa uchache wa mita mbili

# UHIFADHI WA MISITU YA ASILI YA UKANDA WA PWANI

Na Rashid Khamis

Uzinduzi wa mradi wa Uhifadhi wa Misitu ya Asili ya Ukanda wa Pwani uliofanyika Bwawani Hoteli hapa Zanzibar tarehe 30/05/2011 ambapo Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani la GEF, kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo Duniani la UNDP linasaidia uhifadhi wa Mazingira ya Misitu ya Asili ya Tanzania bara na Zanzibar.

Hapa Zanzibar ipo misitu mitatu ya hifadhi itakayofaidika na mradi huu ambayo ni Jozani, Kiwengwa – Pongwe na Masingini kwa Unguja na msitu wa Ngezi Vumawimbi, Ras Kiuyu na Msitu Mkuu kwa Pemba. Wizara ya Kilimo na Maliasili inachukua juhudi za kunusuru kupotea kwa misitu ya asili ambayo imesheheni miti ya asili na wanyamapori kutokana na maeneo ambayo yalikua yamesheheni misitu ya asili sasa yamebakia na vichaka vitupu. Mfano halisi ni kuadimika kwa miti muhimu katika maeneo ya misitu ya kaskazini Unguja, ambapo hasara ya kutokuwa na misitu imeonekana kutokana na kupungua kwa nishati ya kuni za kupikia majumbani.

Misitu ni benki ya kuhifadhi miti na mimea tofauti yenye uhusiano wa moja kwa moja na maisha ya binaadamu, ustawi wa mazingira tunayoishi na maendeleo ya kiuchumi. Aidha, miti ya dawa, miti adimu aina ya mipapindi na wanyamapori kama vile Popo wa Pemba, Kimapunju na Paa nunga huishi katika misitu ya asili nao ni muhimu kwa maisha yetu ambapo bila ya misitu maisha ya viumbe hawa huwa mashakani.

Misitu ya asili pia ni muhimu kwa kinga dhidi ya majanga ya upepo mkali na urekebishaji wa hali ya hewa na upatikanaji wa mvua. Vile vile inachangia maendeleo ya utalii, kutoa ajira kwa wanavijiji wanaozunguka misitu ya hifadhi, kupatikana kwa vyanzo vya maji ambavyo ni rasilimali kubwa kwa maisha ya mwanadamu kwa matumizi ya majumbani na mahoteli (maji ni uhai). Misitu husaidia kujenga afya kwa uzalishaji wa matunda mfano, mabungo na zambarau.

Nje ya maeneo ya misitu ya hifadhi, ipo misitu iliyozunguka maeneo ya vijijini ambayo ni muhimu kwa kuhifadhiwa. Juhudi za uhifadhi ni vyema zihusishe pande zote mbili, misitu iliyo chini ya usimamizi wa taasisi za Kiserikali na iliyo chini ya wanajamii.

Kutokana na harakati za maendeleo ya mwanadamu, baadhi ya maeneo ya misitu ya asili yameanza kupoteza uasili wake kutokana na athari za kukatwa ovyo kwa matumizi ya nishati ya kuni, makaa, kilimo, chokaa, majumba ya kuishi na vitega uchumi.



Daraja la mikoko la Jozani-Pete ni miongoni mwa kivutio cha watalii katika uhifadhi wa msitu wa ukanda wa pwani.

Hivyo, kutokana na kutoweka kwa misitu ambayo ni muhimu katika maisha ya viumbe, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kushirikiana na washirika hao imezindua mradi huo kwa lengo la kuhifadhi misitu pamoja na rasilimali ziliomo kwa faida ya wanajamii na taifa kwa jumla.

Miongoni mwa changamoto zinazosababisha uharibifu wa misitu ni pamoja na kuendelea kupungua kiwango cha maji ardhini ambacho kimepelekea kupungua kwa maji katika visima, mito na kukauka kwa vyanzo vyengine. Kuongezeka kwa kiwango cha joto na kurundikana kwa hewa mkaa. Athari za changamoto hizo husababisha ardhi kukosa rutuba ya kustawisha mazao ya kilimo kunakopelekea uzalishaji mdogo, ukame na njaa kwa binadamu, kufa kwa mifugo, kupotea kwa wanyamapori na kutokea kwa mafuriko wakati wa mvua.

i. Hatua za kuchukua ili kuimarisha uhifadhi wa misitu na kuwa endelevu ni:

ii. Kutenga maeneo zaidi ya uhifadhi wa misitu ya asili na kuimarisha iliyopo,

iii. Kuendeleza taaluma ya uhifadhi wa misitu kwa jamii,

vi. Kufanya ukaguzi wa misitu na kuchukua hatua za kisheria kwa wanaoharibu misitu.

v. Kushirikisha jamii katika uhifadhi kwa kuwasaidia kuanzisha na kuendeleza vitalu vya miti na kupanda miti mingi mjini na vijijini.

vi. Kuacha kuwinda wanyama kiholela pamoja na,

vii. Kuanzisha sheria ndogo ndogo.

Jamii inashauriwa ipunguze kiwango kikubwa cha kuvuna misitu ya asili kwa matumizi ya nishati ya kupikia majumbani, mahotelini na katika mabekari na uchomaji wa chokaa na makaa. Aidha, wanajamii wanatakiwa waendeleze juhudi za kupanda miti ya misitu na matunda na waachane na tabia ya kukata misitu ya asili ovyo, kwani tabia hiyo inasababisha kutoweka miti mikubwa ambayo ni muhimu kwa uzalishaji wa mbegu.

Ushirikishwaji wa wanavijiji katika kufanikisha utekelezaji wa mradi huu unahitajika ili waweze kutoa michango yao katika kupanga na kutekeleza kazi za mradi kupitia kamati zao za uhifadhi misitu. Mradi unapaswa uwashirikishe uongozi wa Wilaya husika katika utekelezaji wake na kuwapatia taaluma ya kupanga na kusimamia uhifadhi wa misitu katika ngazi za Shehia hadi Wilaya.

Vile vile Taasisi za kiserikali chini ya Wizara husika ziunganishe nguvu zao pamoja kupiga vita uharibifu wa misitu na kuhimiza upandaji miti na kuitunza iliyopo iweze kuimarika. Miongoni mwa taasisi hizo ni zinazohusika na Maji, Mazingira, Ardhi na Utalii kushirikiana katika kupanga utekelezaji wa mradi huu.

Katika kuendeleza mradi huu ushirikiano wa pamoja unahitajika baina ya Wizara ya Kilimo na Maliasili Zanzibar na Wizara ya Maliasili na Utalii ya Tanzania bara kupitia Idara ya Misitu na Nyuki, Tanzania unahitajika ili kufanikisha mpango wa utekelezaji wake.

# UFUGAJI BORA WA KUKU WA KIENYEJI

Na Shauri Haji

Ufugaji wa kuku ni mradi ambao hufanywa na wanawake wengi karibu katika kila nyumba hasa vijijini kwa lengo la kupata nyama na mayai kwa ajili ya kitoweleo, kuimarisha afya za familia na kujiongezea kipato. Kuku ni lazima watunzwe vizuri ili watoe mazao bora na kufikia lengo lililokusudiwa.

Ufugaji wa kuku wa kienyeji ni moja ya kazi zinazofanywa na kinamama ambao wameunda vikundi na kupatiwa taaluma za ufugaji bora kupitia Programu za Kuendeleza Huduma za Kilimo na Mifugo kwa wakulima na wafugaji (ASSP/ASDP-L) ya Wizara ya Kilimo na Maliasili hapa Zanzibar. Taaluma hizi za ufugaji zinawasadia wafugaji wa visiwa hivi ambao wengi wao ni wanawake kuongeza uzalishaji, pato na kupunguza umasikini.

Bi. Zeyana Ali Saidi mwenye umri wa miaka 50 ambae ni mkaazi wa kijiji cha Taifu Wilaya ya Wete Pemba, maarufu kwa jina la "Zeyana viponi" ni miongoni mwa wafugaji wa kuku waliopatiwa mafunzo ya ufugaji kupitia programu za ASSP/ASDP-L. Alisema; "Siku za nyuma ufugaji wa kuku haukuwa na tija kutokana na kukosa taaluma ya ufugaji bora na pia ulihitaji kutumia muda mwingi ili kupata mafanikio".

Moja kati ya mambo anayojivunia ni kutengeneza nyumba yake pamoja na kuwasomesha watoto wake kutokana na mauzo ya kuku. Hivi karibuni aliuza kuku 80 ambao walimpatia jumla ya shilingi 400,000/=. Watu wengi wanafuga kuku lakini hawaelewi kanuni na miiko ya ufugaji hivyo bi. Zeyana Ali Saidi yuko mstari wa mbele katika kuwafundisha wafugaji wenzake kulisha chakula bora, kuweka usafi wa mabanda ya kufugia kuku na vifaa, kuwapatia chanjo na matibabu vifaranga na kuku ili kuzuia magonjwa ya mripuko kama mahepe ambayo yanaua kuku wengi yanapotokea. Aidha, anasisitiza kuwa mfugaji anapaswa kufanya usafi wa banda kila baada ya siku mbili kwani usafi hupunguza uwezekano wa kutokea kwa maradhi.



Kuku wa kienyeji hukuwa vizuri na kutoa mazao mengi ikiwa watapatiwa matunzo bora

Mbali na uuzaji wa kuku bi. Zeyana pia ana mpango wa kuuza vifaranga kwa wafugaji wenzake ili kuimarisha soko la kuku wake. Hii itawezekana kwa kutumia mpango maalumu wa utagaji (Program hatching). Njia hii inamfanya kuku mmoja kutaga mara nne kwa mwaka na kuzalisha zaidi ya vifaranga 48 ambapo mfugaji anapata faida zaidi badala ya njia ya kawaida ya uzalishaji vifaranga 20 - 24 kwa ufugaji usiozingatia utaalamu. Vifaranga vinavyototolewa kwa mpango maalumu wa utagaji huingizwa kwenye sanduku lenye uwezo wa kuchukua vifaranga 200 au zaidi na kulelewa kwa muda wa siku saba ambapo hutoa fursa kwa makoo waliototoa kukutana tena na majogoo baada ya muda mfupi.

Njia nyengine ni kutumia koo linalokubali kulea vifaranga hata kama sio wa kwake mradi tu wawe na umri unaolingana.

Miongoni mwa changamoto anazokabiliana nazo ni pamoja na bei kubwa ya madawa na vyakula.

Ili kukabiliana na changanamoto ya upatikanaji wa chakula, wfugaji wanashauriwa kutumia vyakula vinavyopatikana katika mazingira yao na kuchanganya wenyewe majumbani kwao kwa kutumia taaluma waliyapta katika mafunzo.

# TUHAMASISHANE KUPANDA MINAZI YA ASILI

Na Neema A. Khalfan

Mnazi una matumizi mengi hapa visiwani na duniani kote, matumizi hayo ni kama madafu kwa kinywaji, nazi kwa ajili ya kupata tui la kupikia na mbata kwa ajili mafuta ya nazi, makumbi kwa ajili usumba na kamba, makuti hutengenezewa fagio, mapakacha na kuezekea majumba, kigogo cha mnazi pia hutumika kwa mbao, kuni na nguzo za kujengea na pia una matumizi mengine mengi.

Mnamo miaka ya 1970 zao la nazi lilikuwa na upungufu mkubwa ambapo kila mnazi ulitoa wastani wa nazi 23 tu kwa mwaka badala ya uzazi wa kawaida wa nazi 40 kwa mwaka. Uzazi huo ni chini ya wastani wa kiwango cha uzalishaji wa kawaida wa nazi 40 kwa mwaka ambayo ilisababisha upungufu mkubwa wa nazi kwa matumizi ya majumbani na viwandani.

Utafiti uliofanyika uligundua sababu za upungufu wa zao hilo ni kuzeeka kwa minazi ya asili ambapo asilimia 70 ya minazi ilikua ina umri zaidi ya miaka 100 na haikua na uzazi wenye tija, kuwepo kwa wadudu waharibifu, ukosefu wa mafunzo ya kilimo bora cha minazi na uhaba wa ardhi kwa ajili ya utanuzi wa mashamba ya minazi.

Kutokana na upungufu huo mnamo mwaka 1979/1980 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilianzisha Mpango wa Taifa wa Uendelezaji Minazi (NCDP).

Wizara ya Kilimo Zanzibar nayo iliandaa mikakati ya uhamasishaji wa upandaji minazi kwa kutoa mafunzo kwa wakulima juu ya uchaguzi wa mbegu bora, uoteshaji wa miche vitaluni, upimaji, ukaguzi wa mashamba pamoja na usambazaji wa miche.

Mpango huo ulifanikiwa kwa kufanya kampeni katika Wilaya za Magharibi, Kaskazini A, Kaskazini B, Kati na Kusini kwa Unguja sambamba na kuwapa wakulima ushauri, mafunzo ya kupanda miche chini ya minazi mikongwe na kuwashauri kutumia vipimo vinavyotakiwa (mita 10 kwa 15) kutoka mnazi hadi mnazi bila ya kujali msongomano uliopo shambani mpando huu ulisaidia uendelezaji wa upatikanaji wa mavuno huku ikisubiriwa miche iendelee na ukuaji wake.



Minazi iliyopandwa katika masafa yaliyopendekezwa na wataalamu hurahisisha palizi, kutoa mavuno bora na kumpa fursa mkulima kuchanganya na mazao mengine

Jumla ya wakulima 250 walihudhuria katika kampeni hiyo na wakulima 102 walikaguliwa mashamba yao ambapo mashamba 47 yalikaguliwa, 22 kipindi cha Vuli na 25 Masika, wakulima 20 walipimiwa mashamba yao na kupatiwa miche.

Katika kipindi cha Vuli 2010 na Masika 2011 Wizara ya Kilimo na Maliasili kupitia vitengo vyake vya uzalishaji wa miche ya minazi imefanikiwa kuzalisha na kuiuza kwa wakulima miche ya minazi ya asili 10,260.

**Upunguzaji wa Minazi Mikongwe**

Wizara iliendelea na juhudi za kuwashajiisha wakulima kupunguza minazi mikongwe katika mashamba yao kwa kupanda minazi mipya chini ya minazi hiyo na baada ya miaka mitatu ya ukuaji, walishauriwa kukata minazi mikongwe na kuondoa magogo kwa lengo la kuzuia mazalia ya chonga. Aidha, wakulima walisisitizwa kuondoa magogo yote yaliyomo shambani na kuyatumia kwa kuchoma chokaa, kupasua mbao, kujengea daraja ndogo ndogo za kuvukia, vibao vya kukalia na kuni.

**Uchaguzi wa miche**

Inashauriwa kuchagua miche iliyobora kwa ajili ya upandaji. Miche bora huwa na sifa ya kukua haraka na kutoa mazao bora. Miche bora ni ile ambayo haikushambuliwa na wadudu au magonjwa, yenye afya na majani yake yasipungue sita (6) na yawe kijani iliyokooza na imekaa kitaluni kwa muda usiopungua miezi tisa (9).

**Uchimbaji wa mashimo**

Inashauriwa kuchimba mashimo yenye urefu, upana na kina cha sentimita 60 (futi mbili), udongo wa chini utenganishwe na wa juu ambao mara nyingi huwa na rutuba, baadae uchanganywe na mbolea za kienyeji kama vile samadi na mboji debe moja au ndoo moja. mbolea hizi hupatikana kwa urahisi katika maeneo yetu.

**Upandaji wa miche**

Weka udongo wa juu uliochanganywa na mbolea kiasi katika shimo, panda mche katikati ya shimo, endelea kufukia kwa udongo uliochanganywa na mbolea na kumalizia na udogo wa chini. Hakikisha unalishindilia vizuri shimo lako ili kuzuia mche kung'oka kwa urahisi.

Zao la nazi ni muhimu hapa Zanzibar, hivyo Wizara ya Kilimo na Maliasili inaendelea kuielimisha na kuishajiisha jamii kupanda minazi ya asili ili zao hili liwe endelevu kwa faida ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Kwa maelezo zaidi ya uchaguzi wa miche ya minazi na upandaji wasiliana na mhudumu wa kitalu, muone bwana/bibishamba wako au mtaalamu wa kitengo cha minazi uliye karibu nae.

# FAIDA ZA KILIMO CHA MAPESHENI

Na Makame M. Abdulrahman

Pesheni kwa jina la kitaalamu linajulikana Passiflora edulis ni zao lenye asili ya Marekani ya Kusini. Inasadikiwa kwamba pesheni lenye rangi ya manjano lilitokea katika msitu wa Amazon (Brazil) mnamo miaka ya 1900. Hata hivyo zipo taarifa zinazothibitisha kwamba kwa mara ya kwanza mmea huu ulipandwa nchini Hawaii ukitokea Australia mnamo mwaka 1880.

Zao hili ni muhimu katika kukuza biashara na chakula kwa kuwavutia wageni na watalii mahotelini.

Pesheni ni zao linalolimwa sana hapa Tanzania katika maeneo ya Zanzibar, Morogoro, Dar es Salaam, Tanga, Kigoma, Mbeya, Kilimanjaro, Arusha na Mkoa wa Pwani. Hapa Zanzibar mmea huu umeanza kuingia katika miaka ya 80 na kupata umaarufu zaidi katika miaka ya 90. Wastani wa uzalishaji kwa Tanzania ni tani 1,080 kwa mwaka sawa na asilimia 0.1 ya uzalishaji wa matunda yote nchini. Kwa kawaida, mapesheni yana virutubisho bora kwa afya ya binadamu vikiwemo nguvu kilokalori 60, sukari gramu 9.1, vitamini A IU 241, vitamini C miligramu 64.7 na maji gramu 84.2 kwa kila gramu 100.

Mavuno mengi ya zao la pesheni hupatikana iwapo kanuni za kilimo bora zitatekelezwa kwa kuchagua aina bora ya miche ya kupanda kulingana na mahitaji ya soko, kudhibiti wadudu waharibifu na magonjwa, kuondoa magugu na kukagua shamba mara kwa mara iwapo kuna dalili za mashambulizi ili yaweze kudhibitiwa mapema ili kupata mazao mengi na bora. Palizi ni muhimu ili mimea iweze kutumia virutubisho kwa ukamilifu.

Mpesheni ni mmea unaokua kwa kutambaa hivyo katika ukuaji wake ni muhimu kuweka miti ili uweze kutambaa juu yake. Uwekaji wa miti hurahisisha kuhudumia wakati wa kupalilia na kuvuna. Aidha, ukaguzi wa shamba hufanywa ili kuona



Pesheni hutengenezwa juisi ambayo hutumika kama kiburudishaji wakati wa chakula

kama matunda yamekomaa. Kwa kawaida mapesheni hukomaa baada ya miezi miwili hadi mitatu baada ya maua kuchanua. Dalili za mapesheni yaliyokomaa ni kubadilika rangi kutoka kijani kuwa manjano au zambarau kutegemea na aina ya pesheni ambapo hung’ara na kunukia. Kabla ya kuvuna ni vizuri kusafisha shamba na kuondoa magugu chini ya mimea kurahisisha uvunaji na uokotaji wa matunda. Pia inatakiwa kuandaa vifaa vya kubebea kama pakacha, masusu, ndoo, vikapu na vipolo.

Njia bora ya kuvuna mapesheni ni kutumia mikono ambapo matunda huokotwa baada ya kudondoka yenyewe kutoka kwenye mti, matunda yakichumwa yanapokuwa katika mmea hushuka ubora wake, husinyaa au huoza yanapovumbikwa.
Matunda yaokotwe mara mbili kwa siku ili kuepuka kubabuka kwa jua, kuliwa na wadudu na ndege. Matunda yaliyovunwa yawekwe kwenye vifaa na kuhifadhiwa kivulini kabla ya kupelekwa sokoni.

Kabla ya kupeleka sokoni mapesheni huchaguliwa ili kuyaondoa yaliyooza na yaliyoharibika. wakati wa kuchagua ni muhimu kuondoa mapesheni yaliyooza na yenye wadudu yafukiwe ili kudhibiti kuenea kwa wadudu waharibifu na vimelea vya magonjwa. Aidha, matunda yaliyopasuka, kubonyea, kusinyaa na kuchubuka yatumiwe haraka na mazuri yaliyobaki yatumike kwa kusindikwa na kuuzwa.

Mapesheni yahifadhiwe sehemu yenye baridi ya nyuzi joto 5 hadi 13 za sentigredi na unyevu wa asilimia 80 hadi 90 na huweza kukaa kwa muda wa wiki tatu hadi nne bila kuharibika.

**Namna ya kutayarisha Juisi**

Njia nzuri ya kutayarisha juisi ya pesheni ni kuchagua matunda yaliyoiva na kuyasafisha kwenye maji safi na salama, kata matunda na ondoa maganda ya nje, saga pamoja na mbegu za tunda, chuja kwa kutumia kitambaa au chujio safi na weka juisi kwenye chupa safi. Acha nafasi ya milimita 5 kutoka kingo ya mdomo wa chupa na funika kwa vifuniko imara na safi na ihifadhi kwenye sehemu baridi tayari kwa kutumia. Juisi ya mapesheni iliyotengenezwa kwa njia hii huhifadhika kwa miezi sita bila kuharibika.

Jarida la KILIMO

Toleo la Sita
Aprili - Juni, 2011

# MCHANGO WA MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF) KATIKA SEKTA YA KILIMO

Na Shaaban Abdulmalik

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii awamu ya Pili (TASAF II) ulianza kazi mwaka 2006, kwa kuhamasisha na kutoa elimu kwa Jamii kuhusu madhumuni ya Mfuko huo na majukumu ya kila mdau katika utekelezaji wake, ambapo Visiwa vya Unguja na Pemba vinaendelea kunufaika na mfuko huo.

TASAF II ina jukumu la kusaidia jamii masikini katika kuongeza upatikanaji wa matumizi ya huduma za msingi za jamii ili kufikia malengo ya Milenia na kuziwezesha jamii kutumia fursa zilizopo kuomba, kutekeleza na kusimamia miradi yao watakayoichangua ili kuinua hali zao za maisha na hatimae kufikia lengo la Mpango Mkuu wa Kupunguza Umasikini.

Katika kutekeleza mkakati wa Taifa wa kupunguza umasikini nchini, Sekta ya kilimo kupitia TASAF II imepewa kipaumbele, hivyo iliweza kutekeleza jumla ya miradi 27 ambayo ilikuwa na thamani ya shilingi 660,012,552/=. Kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa kunakosababisha kilimo cha kutegemea mvua kuwa si cha uhakika, nguvu kubwa za utekelezaji zilielekezwa katika kilimo cha umwagiliaji maji ambacho ni mkombozi kutokana na hali hiyo.

Aidha katika utekelezaji wa miradi hiyo maeneo ya Bonde la Bumbwisudi nambari tano, Uzini na Mgenihaji, Mchangani, Kianga na Cheju kulianzishwa miundombinu ya kumwagilia maji mpunga. Eneo la Kitogani, Kijini Makunduchi, Mzuri, Jendele, Dunga, Mpapa, Matetema na Zingwezingwe kumeanzishwa miundombinu ya umwagiliaji maji kwa njia ya matone katika kilimo cha mbogamboga.

Miradi mingine ya uhifadhi wa mazingira na upandaji wa miti imetekelezwa katika



Katibu Mkuu, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar Dkt. Khalid S. Mohamed anaechimba mtaro akizindua mradi wa miundombinu ya umwagiliaji maji Bumbwisudi

maeneo ya Kianga, Kikobweni, Kandwi na Matemwe. Kazi ya utekelezaji wa miradi katika maeneo haya ilinufaisha zaidi ya wakulima 1000.

Uhamasishaji na upelekaji wa fedha kwa jamii kwa ajili ya utekelezaji wa miradi, mafunzo ya usimamizi wa miradi, uwekaji wa kumbukumbu, utunzaji wa fedha, mipango ya biashara na kuweka na kuwekeza yalifanyika kwa jamii. Mafunzo hayo yamenufaisha Shehia 172 za kisiwa hiki, ni mategemeo yetu kuwa yataifaidisha Jamii katika utekelezaji wa miradi yao ya maendeleo kwa sasa na baadae, Pia mashirikiano baina ya TASAF na mradi wa kuimarisha huduma za Kilimo yameimarisha zaidi ya vikundi 200 vya Skuli za wakulima Unguja.

Katika usimamizi na utekelezaji wa kazi za miradi ya jamii, ni vyema kuwepo kwa wataalamu mahiri wa kusimamia miradi, iandaliwe mapema na kwa uhakika ili itoe matunda bora. Kuhakikisha tathmini zimefanywa vizuri kuhusu kuwepo kwa wachangiaji na michango inapatikana kwa wakati. Uratibu na mashirikiano kwa programu zinazofanana au miradi inayohitaji wataalamu kutoka sekta tofauti ni jambo muhimu sana. Hata hivyo, changamoto kubwa baada ya wananchi kufurahia utaratibu shirikishi wa utekelezaji wa Miradi ya TASAF na matunda yake kumeonekana ni kwamba tunaweza kutanua wigo na kuudumisha mpango huu.

Kumalizika kwa kazi ya upelekaji wa fedha za utekelezaji wa miradi kwa wanajamii, hakujabadilisha majukumu ya msingi ya Halmashauri zetu, Sekta na Taasisi husika katika kusimamia mwenendo wa miradi hiyo kitaalamu, kisiasa na kiuchumi na kuhakikisha uendelevu wake. Ili kufikia mikakati tuliyojiwekea ya kupunguza umasikini tunahakikisha kuwa fedha za mkopo zilizotolewa zinaleta manufaa kwa wananchi na nchi yetu.

GAZETI HILI HUTOLEWA KILA BAADA YA MIEZI MITATU NA
WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI - ZANZIBAR
P. O. Box 159 Zanzibar, Simu: +255 24 2230986, Fax: +255 24 2234650
Barua pepe: kilimo@zanlink.com, Tovuti: www.kilimoznz.or.tz